

**KUWEKA WATOTO WAKFU NI TENDO LA**  
**UFAHAMU WA HALI YA JUU SANA**  
**WA KIROHO KWA WAZAZI.**

**Maandiko: MARK. 10: 13 – 16**

**1. UTANGULIZI:**

Kuweka watoto wetu wakfu (kuwabariki) ni tendo kubwa sana la imani lenye maana ya kuwatenga watoto hao tangu wanapokuwa watoto wadogo kuwa mali ya Bwana Yesu; ni tendo la kutangaza kwa vitendo tena hadharani kwamba mtoto wangu tangu leo siyo mali ya dunia au mali ya dini au mali yetu sisi wazazi tuliomzaa, bali ni mali ya Bwana Yesu mwenyewe!!! (ni mali ya Mungu)

- Na mimi Kuhani wa Bwana Yesu nafurahia kufanya tendo hili la kuweka watoto wadogo wakfu (kuwabariki) kwa sababu naamini kwamba tangu siku hii ya leo ninapowabariki; wataanza kuishi pamoja na kukua na kuongezeka nguvu zao za rohoni kwa uangalizi wa Yesu Kristo mwenyewe kwa sababu wazazi wamemkabidhi yeye Yesu Kristo watoto wao ili wawe mali yake tangu wanapokuwa watoto wadogo. ***1Samwl. 2: 26, Mith. 3:1- 4. Kwangu mimi kufanya kazi ambayo angeifanya Yesu Kristo mwenyewe ni heshima kubwa sana ambayo kibinadamu nisingestahili kabisa.***
- Hiki ni kitendo ambacho mbingu zinakiheshimu mno mno mno; na Yesu Kristo anawathamini sana Wazazi waliowaleta watoto wao kwake ili wawe mali yake yeye aliye na mamlaka ya kuwalinda na kuwakuza na kisha kuwaandaa kuwa watu wakuu baadaye.

**2. Umuhimu wa kuweka watoto wetu wakfu.**

- a. **Kama ilivyokuwa katika Math. 2: 2, 9 – 11, mtoto ndiyo nyota katika familia yoyote, wazazi wengi wanaweza kuwa na ndoto au maono ya kufanya mambo Fulani kuhusu Mungu na Taifa kwa ujumla; lakini**

**watoto wao ndiyo watakaokuja kutimiza ndoto hizo pamoja na maono hayo makubwa walio nayo leo. 2Samwl. 7: 12 – 14, Isay. 11: 1-3.**

**Mfano:-**

- i. Mzee Tera** (Baba yake na Abrahamu) hakufahamu kwamba amezaa **nyota** ambayo itakuwa sababu ya familia yake iliokuwa inaabudu miungu ya kipagani imjue Mungu wa kweli na hatimaye Mungu afanye Agano na yeye la kuwa Taifa kubwa hadi leo!!! **(Mwz. 12: 1-8. Mwanzo 22: 15 – 18.**
  - ii. Au Mzee Yakobo na mkewe Raheli** - Wakati wamemzaa mtoto wao Yusufu, hawakufahamu kabisa kwamba wamezaa **NYOTA** ambayo baadaye itakuwa sababu ya Familia yake yote kupata wokovu na kutokufa kwa njaa kali iliyoua mataifa mengine!!! **Mwanz. 45: 8-20, 47:11 - 12**
  - iii. Au mzee Amramu na mkewe Yokebedi;** walipomzaa mtoto wao Musa, hawakufahamu kabisa kwamba Musa ndiye **nyota** ya Familia yao pamoja na wokovu mzima wa Taifa la Israeli. **Kut. 2: 1-4, Kut.6:20 na Hes. 26: 59**
  - iv. Au Mzee Elikana na Mkewe Hana.** Walipomzaa mtoto Samweli; hawakufahamu kabisa kwamba Samweli ndiye **nyota** katika familia yao na Taifa la Israeli kwa ujumla atakayekuwa **Nabii** na **Mwamuzi** wa Taifa la Israeli kwa weledi mkubwa!!! **1Samwl. 3: 19-20**
  - v. Au Mzee Yese;** alipomzaa mtoto Daudi, hakufahamu kabisa kwamba mtoto Daudi ndiye atakayekuwa **NYOTA** ya familia yake na baadaye kuwa mtiwa mafuta na Mfalme maalumu sana wa Taifa la Israeli; yeye aliona kuwa amezaa kachunga kondoo tu!!! **1samwl. 16: 11- 13.**
- b. Tunaweka watoto wakfu na kuwatamkia maneno makuu na Baraka; maneno hayo yanayotamkwa juu ya watoto hao ndiyo yatakayobeba sura halisi ya maisha yao ya

baadaye kwa kadri watakavyoendelea kukua na kuongezeka. **Mwanz. 27: 27 – 29, Mwanz. 48: 13 – 20, Luk. 2: 25 – 38.** Kabla ya laana ya Torati, watoto waligombania sana matamko ya wazazi wao.

- c. **Kuwaweka watoto wakfu** (kuwabariki) ni tendo la imani ambalo linabeba tangu siku hiyo **ulinzi wa watoto hawa muda wote wanapokuwa hapa duniani, na ni tendo ambalo linasababisha waanze kukua na kuongezeka katika hekima na maarifa ya Mungu na kuwafanya wamche Mungu popote watakapokuwa hata kama hawako machoni pa wazazi wao. Mith. 3: 1 -4.**
- d. **Tunapowaweka watoto wakfu** (kuwabariki) tunafanya pia tendo la imani sana la kuiambatanisha mioyo ya watoto ili iambatane na mioyo ya wazazi wao!!! **Malaki 4:4.** Hii ni siri kubwa ya kiroho tuliyo nayo sisi watumishi halisi wa Mungu.

“Sisi sote tunafahamu kabisa kwamba hakuna mzazi yeyote asiyetaka kufanana na mtoto/ **watoto wake kwa sura, kwa tabia na hata kiroho pia, na Mungu kwa uaminifu wake kabisa anapowaona wazazi makini ambao wanawaleta watoto wao ili wabarikiwe (wawekwe wakfu) kwa siri kubwa na kwa uweza wake alionao wa Uumbaji, anaunganisha mioyo ya watoto na wazazi wao ili waweze kumtumikia Mungu kwa pamoja tena wakiwa na mioyo ya furaha.**

- Hizi ndizo sababu zilizomfanya Yesu awakumbatia watoto na kuwabariki; **Mark. 10: 13 – 16. Amina.**

**Na**  
**Ask. Dr. L. M. Mwizarubi**  
**26/12/2022**